# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

**Mawasiliano:**
Simu: 0732973257
Nukushi: 027-2756863
Barua pepe: ded@sihadc.go.tz
Tovuti:www.sihadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
S. L. P. 129,
Sanya Juu,
**SIHA.**

Tarehe: **30/12/2018**

## TAARIFA KWA UMMA

## ZOEZI LA UGAWAJI VITAMBULISHO KWA WAJASIRIAMALI SIHA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha inapenda kutoa ufafanuzi kwa Umma ya Watanzania na Wananchi wa Wilaya ya Siha kuhusu taarifa zilizotolewa na gazeti la Nipashe la tarehe **29/12/2018** lenye kichwa cha habari ***"VITAMBULISHO 23,500 VYA WAMACHINGA VYAKOSA WATU".***

Kwanza kabisa tunapenda kufahamisha umma kuwa, taarifa hizi ni za uongo na zimelenga kupotosha umma na Wananchi wa Siha na Watanzania kwa ujumla kuhusu zoezi la ugawaji wa vitambulisho Wilayani Siha,Ukweli ni kwamba Wilaya ya Siha imepangiwa na kukabidhiwa vitambulisho **1,500** tu na siyo **25,000** kama ilivyoripotiwa katika gazeti tajwa hapo juu. Idadi ya vitambulisho **25,000** ni vitambulisho vyote kwa ajili ya **Mkoa wa Kilimanjaro** na siyo idadi kwa ajili ya Wilaya ya Siha.

Hata hivyo,Wilaya ya Siha imezindua zoezi la ugawaji vitambulisho kwa wajasiria mali **tarehe 27/12/2018** ambapo siku ya uzinduzi jumla ya vitambulisho **900 kati ya 1500** vilitolewa na **Mhe. Onesmo Buswelu** Mkuu wa Wilaya ya Siha kwa wajasiriamali wadogo wadogo waliopo katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Siha.Hadi leo tarehe **30/12/2018** zoezi linaendelea vizuri na mategemeo ya Wilaya ya Siha ni kuhakikisha vitambulisho **vyote 1500** vinatolewa hadi kufikia wiki ya pili ya **mwezi Januari 2019.**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji inawaomba wananchi na Umma ya Watanzania kuzipuuza taarifa za upotoshaji zilizotolewa kwani kimsingi zinaonesha kuwa watoa taarifa walikuwa na malengo ya kupotosha umma kuhusu mafanikio ya zoezi la utoaji wa vitambulisho kwa wamachinga linaloendelea vizuri katika Wilaya yetu.

Mwisho, tunapenda kuwaomba na kuwakumbusha waandishi na vyombo vya habari kuzingatia misingi ya taaluma ya uandishi wa habari ili kuepuka kutoa taarifa zisizo sahihi kwa umma kwani mara nyingi zinasababisha usumbufu na taharuki kwa jamii. Tunawaomba tuendelee na ushirikiano wa kuhabarisha umma katika mambo mbalimbali ya maendeleo.

Imetolewa na

**Zakayo E. Mosha**

Mkuu wa Kitengo cha Habari & Mawasiliano (W) Siha

**Tarehe 30 Desemba, 2018**